



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

MWALIKO WA WATAZAMAJI WA UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE JIMBO
LA ARUMERU MASHARIKI NA UDIWANI KATIKA KATA SITA (6)
UTAKAOFANYIKA TAREHE 19 MEI, 2019

Kwa mujibu wa kifungu cha 37 (1) (b) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 13 (3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kuendesha Uchaguzi Mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Arumeru Mashariki na Udiwani katika Kata sita (6) kwenye Halmashauri sita za Tanzania Bara, kwa ajili ya kujaza nafasi wazi zilizotokana na kupoteza sifa, kujiuzulu na vifo.

Kwa ajili ya kuweka uwazi katika Uchaguzi huo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuzingatia Kanuni ya 18 (2) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2015, na Kanuni ya 14(2) ya Kanuni za Uchaguzi wa (Madiwani) za mwaka 2015, inapenda kualika Asasi za Kiraia na Taasisi mbalimbali za ndani zinazotaka kuwa Watazamaji wa Uchaguzi katika Uchaguzi Mdogo unaotarajiwa kufanyika tarehe **19 Mei, 2019**.

Asasi/Taasisi zinapaswa kuzingatia masharti yafuatayo wakati wa kuwasilisha maombi yao:-

- (i) Anuani Kamili ya Taasisi husika,
- (ii) Anuani ya Makazi ya Ofisi ya Taasisi husika ilipo,
- (iii) Shughuli ambazo zinafanywa na Taasisi husika kwa mujibu wa Hati ya Usajili
- (iv) Kutaja sehemu ambazo Asasi/Taasisi inataka kufanya zoezi hilo la Utazamaji.

- (v) Kutaja idadi ya watu ambao Taasisi / Asasi itawatumia katika zoezi hilo pamoja na taarifa zao.
- (vi) Kutaja majina na namba za simu za viongozi wa Taasisi husika kama yalivyoandikwa katika Hati za Usajili wa Taasisi.
- (vii) Ikiwa Taasisi inahusisha Watendaji wa Kimataifa wawili lazima wawe watanzania.
- (viii) Kuambatanisha nakala/kivuli cha hati ya Usajili wa Taasisi husika.
- (ix) Kuambatanisha nakala / kivuli cha Katiba ya Taasisi / Asasi husika.

Vilevile, Taasisi zitakazopewa vibali vya kuwa Watazamaji zitapaswa kuzingatia Mwongozo kwa watazamaji wa ndani na wa Kimataifa ulioandaliwa na Tume kwa mujibu wa kanuni ya 24 ya kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge na Kanuni ya 20 ya Kanuni za Uchaguzi wa Madiwani za mwaka 2015

Maombi ya kuwa Watazamaji wa Uchaguzi yatapaswa kuwasilishwa kwa maandalizi Tume ya Taifa ya Uchaguzi Makao Makuu kuanzia tarehe 11 hadi 17 Aprili 2019 kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Uchaguzi,
Tume ya Taifa ya Uchaguzi,
Posta House, Ghorofa ya 7,
Mtaa wa Ghana/Ohio,
S. L. P. 10923,

DAR ES SALAAM.

Jimbo litakalofanya Uchaguzi Mdogo.

NA.	JIMBO	Na.	HALMASHAURI	NA	MKOA
	Arumeru Mashariki		Wilaya ya Meru		Arusha

Kata zitakazofanya Uchaguzi Mdogo.

NA	KATA	NA	HALMASHAURI	NA	MKOA
1.	Mikocheni		Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni		Dar es salaam
2.	Kitobo		Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi		Kagera
3.	Uwanja wa Ndege		Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda		Katavi
4	Kyela		Halmashauri ya Wilaya ya Kyela		Mbeya
5.	Mvuleni		Halmashauri ya Wilaya ya Lindi		Lindi
6.	Manda		Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino		Dodoma

Ratiba ya Uchaguzi huo ni kama ifuatavyo:-

Na.	Tukio	Tarehe
1.	Kutoa Fomu za Uteuzi	15 - 19 Aprili, 2019
2.	Siku ya Uteuzi wa Wagombea	19 Aprili, 2019
3.	Kampani za Uchaguzi	20 Aprili, 2019 hadi 18 Mei, 2019
4.	Siku ya Kupiga Kura	19 Mei, 2019

IMETOLEWA NA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI